


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Nukushi: +255 25 295 7391
Simu Na: +255 25 295 7388
Barua pepe: td@tundumatc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P 73,
TUNDUMA - MOMBA
TANZANIA

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

MKURUGENZI WA MJI TUNDUMA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA ZILIZOANISHWA KWENYE TANGAZO HILI KUOMBA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI.

WAKUSANYA MAPATO (NAFASI 40)

MAJUKUMU YA KAZI.

1. Kukusanya Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia mashine za kielectronic za kukusanyia Mapato (POS)
2. Kuhakikisha Fedha inayokusanywa inapelekwa bank kwa wakati
3. Kuhakikisha Mapato yote yanayopaswa kukusanywa na Halmashauri yanakusanywa kwa usahihi

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye elimu ya kuanzia kidato cha nne na kuendelea ambao wana uelewa wa kutumia simu ya tachi, sababu Mapato yote ya serikali yanakusanywa kwa kutumia mashine za kielectronic za kukusanyia Mapato (POS) ambayo ina application sawa na simu za tachi.

MASHARTI YA WANAOMBAJI KATIKA KAZI HII

1. Awe ni raia wa Tanzania, Umri kuanzia miaka 21
2. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa
3. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anwani na namba simu za kuaminika pamoja na Majina mawili ya wadhamini (**Referees**) na anwani zao sahihi na Namba za simu.
4. Maombi yaambatane pamoja na nakala ya vyeti vyote vya kitaaluma vya mwombaji
5. Awe tayari kupangiwa kituo chochote cha kukusanya Mapato ndani ya Mji wa Tunduma
6. Awe Muaminifu katika kukusanya Mapato ya serikali na kuhakikisha fedha ya serikali haiptei.
7. Awe tayari kutii na fuata maelekezo atakayopangiwa bila kuvunja misingi ya Sheria ndogo za Halmashauri.

BARUA ZA MAOMBI ZITUMWE KUANZIA LEO 21.05.2021 NA MWISHO WA KUPOKEA BARUA ZA MAOMBI HAYO NI TAREHE 10.06.2021. WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA WATUME MAOMBI YAO KWENYE ANWUANI IFUATAYO:

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA
S.L.P 73
TUNDUMA



Lusajo Mwalukasa

KAIMU MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
TUNDUMA

